




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA)**



**HAFLA YA UFUNGUZI WA NYUMBA 644
ZA WAKAAZI WA MAGOMENI KOTA KINONDONI JIJINI
DAR ES SALAAM MACHI 23, 2022**



Proudly Housing Public Servants in Tanzania



Msafara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ukiwasili kwenye Hafla ya Ufunguzi wa nyumba 644 zilizojengwa na Serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika eneo la Magomeni Kota.





Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisalimiana na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi **Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb)** mara baada ya kuwasili kwenye Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) **Bw. Ludovick J. Nduhiye** mara baada ya kuwasili kwenye Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za Magomeni Kota.



Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifuatilia wasilisho la ubunifu wa Nyumba 644 za Makazi za Magomeni Kota lililowasilishwa na Mtendaji Mkuu wa TBA Arch. Daud W. Kondoro.



Rais wa Jamhuri ya Muungano ya **Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan** akisoma jiwe la ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan** akiwakabidhi **Bibi. Mwajuma Sama** na **Mzee Henry Ngwemba** mfano wa ufunguo kama ishara ya kuwakabidhi rasmi nyumba wakaazi 644 wa **Magomeni Kota.**

Proudly Housing Public Servants in Tanzania

7



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan** akielekea jukwaani baada ya kukagua nyumba 644 zilizojengwa na Serikali kupitia **Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)** katika eneo la **Magomeni Kota** Jijini Dar es Salaam wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa nyumba hizo.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan** akizungumza na hadhara iliyohudhuria kwenye Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za Magomeni Kota.

Proudly Housing Public Servants in Tanzania

9



Akizungumza katika hafla hiyo Mhe. Rais Samia amesema “nimefurahishwa zaidi na ubunifu na hekima iliyotumika kupambana na changamoto mbalimbali lakini mradi wa ujenzi wa nyumba hizi ukamilike. Nakushukuru sana Mtendaji Mkuu wa TBA **Arch. Daud Kondoro** kwa ubunifu na hekima uliyotumia. Hatua hii ya ujenzi wa nyumba za maghorofa katika mradi huu ni utekelezaji wa sera ya matumizi bora ya Ardhi ya kutekeleza ujenzi wa nyumba za kutosha kweye maeneo ya umma ili wananchi wengi waweze kunufaika na miradi hii. Najua changamoto nyingi zilijitokeza kama nilivyosema juhudi kubwa zimefanywa kupambana na changamoto hizo hadi mradi huu leo kukamilika na kuja kufunguliwa”



Vile vile Mhe. Samia, ametoa maelekezo kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuruhusu wananchi wa Magomeni Kota kuuziwa nyumba kwa utaratibu wa mpangaji mnunuzi. Wakazi hao ambao wameahidiwa kukaa bure kwa miaka mitano, wameruhusiwa kulipa gharama za ujenzi wa nyumba pekee bila ya gharama za ardhi na miundombinu ya jumuiya baada ya miaka hiyo. Pia kwa wakaazi wanaotaka kulipa gharama ya ununuzi kabla ya kufika miaka mitano wanaruhusiwa kulipa kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka 10 bila ya riba yoyote.

Rais Samia amewasihi wakaazi hao kutunza nyumba hizo na kuzingatia usafi wa ndani na nje na kuchangia huduma jumishi kwa faida ya kila mmoja. Ambapo alisema. "Mimi ninawaomba matunzo ya hizi nyumba, kwa sababu nyumba hizi wako wengi watakuwa wanakaa humo ndani. Usafi unaweza kuwa changamoto. Hivyo tengenezeni kamati ambazo zitasimamia usafi wa hizi nyumba. Pamoja na kwamba TBA watakuwa wanatoza gharama za usimamizi wa mitambo, Lifti na mambo mengine kwa ajili ya uendeshaji wake. Lakini Usafi wa nyumba ni jukumu lenu naomba sana muwe wasafi na mazitunze."





Katika Hafla hiyo Mhe. Kakoso amemuomba Mhe. Rais kuendelea kuwaangalia TBA kwa kuwapatia fedha za kutosha zitakazowasaidia kuweza kujenga maeneo ambayo tayari walishaandaa kwa ajili ya uwekezaji. “TBA asilimia nyingi ya kazi wanazofanya ni za serikali lakini bahati mbaya sana, TBA imekua ni Wakala ambao una matatizo makubwa sana katika ulipwaji wa wale ambao umewafanyia kazi, taasisi nyingi zikijengewa au zikipanga kwenye nyumba za TBA hawalipi” amesema Mhe. Kakoso.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu **Mhe. Selemani Kakoso (Mb)** akizungumza na hadhara iliyohudhuria kwenye Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.





Prof. Makame Mbarawa
Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi

Akizungumza katika Hafla hiyo, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Makame Mbarawa amewashukuru wadau wote walioweza Mradi wa Ujenzi wa Nyumba 644 za Mkaazi za Magomeni Kota kukamilika kwa ufanisi mkubwa wakiwemo Wakaazi 644 wa Magomeni Kota, Taasisi za Ujenzi zinazoshughulikia sekta ya Ujenzi pamoja na shukrani za pekee kwa TBA na TEMESA waliofanya kazi usiku na mchana kuhakikisha mradi unakamilika kwa asilimia 100.

Pia **Mhe. Mbarawa** amemhakikishia Mhe. Rais juu ya utunzaji wa nyumba hizo. Waziri Mbarawa amesema "Ili kutunza majengo haya wizara yangu kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo Tanzania imeandaa mwongozo ambao umezingatia mambo muhimu yatakayoingizwa kwenye mkataba kati ya TBA na wakaazi. Baadhi yake ni uchangiaji wa huduma jumuishi kama vile usafi, uzoaji wa taka ngumu, ulinzi, maji safi na maji taka, na umeme wa maeneo ya jumuiya ambapo gharama hizo zitatakiwa kuchangiwa na kila mkaazi. Tunategemea kwa kufanya hivi wakaazi watakuwa wameshirikishwa kikamilifu na ili kuendelea kuzipatia nyumba hizi thamani inayohitajika"





Arch. Daud Kondoro

Mtendaji Mkuu - TBA

Awali Mtendaji Mkuu wa TBA **Arch. Daud Kondoro** alielezea namna TBA ilivyotekeleza mradi huo kwa kufanya ubunifu ambao ulizingatia Uwepo wa mabadiliko ya maisha ya wakazi wa eneo hili kabla ya uhuru na baada ya uhuru ambapo wakati huo familia zao zilikuwa ndogo (Bachelor) na walihitaji mahitaji ya kawaida na majengo hayakuwa na miundombinu, Mahitaji ya familia kuongezeka baada ya Uhuru kutokana na kutokuwepo na Mpango Maalum wa kuboresha makazi yao hatimaye nyumba za Wakaazi hawa ziliharibika vibaya na kuwa si salama kuishii pamoja na Ukuaji wa uchumi na uboreshwaji wa miundombinu ulioifanya ardhi ya eneo hili kuwa na thamani kubwa.

Pia **Arch. Kondoro** alitoa ufafanuzi juu ya uwekezaji mwingine uliofanywa na TBA katika eneo hilo la Magomeni Kota ambapo alisema “Katika kuungana nawe kwenye jitihada zako na kwa kuzingatia kuwa eneo hili linakadiriwa kuwa litakuwa na watu takribani elfu tatu (3,000), TBA iliamua kuanzisha miradi mingine kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani kwa kuanza kujenga majengo ya kibiashara yatakayotoa huduma kwa wakaazi watakaoshi katika eneo hili na maeneo jirani. Miradi hiyo inajumuisha soko la wafanyabishara wadogo wadogo maarufu kama machinga” ambapo eneo hilo lina ukubwa wa mita za mraba 3,500 ambalo limegawanywa katika maeneo madogo madogo (Vizimba) kulingana na biashara itakayohusika. Kwa eneo hili kumepatikana jumla ya vizimba 186 vyenye ukubwa wa mita za mraba 9 kila kimoja.



Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika picha ya pamoja na kamati ya maandalizi ya **TBA** wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na sehemu ya menejimenti ya **Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)** wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Baadhi ya wageni waalikwa waliohudhuria Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Baadhi ya wakaazi wa **Magomeni Kota** waliohudhuria Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Mussa Zungu** akijadiliana jambo na Mtendaji Mkuu wa TBA **Arch. Daud Kondoro** kabla ya hafla ya ufunguzi wa nyumba 644 za makazi za **Magomeni Kota**.

Proudly Housing Public Servants in Tanzania

17



Muonekano wa picha ya juu ya mradi wa ujenzi wa Nyumba 644 za Makazi za Magomeni Kota ambao umegharimu kiasi cha fedha kiasi cha shilingi Bilioni 52.195.

MAGOMENI KOTA MACHINGA CENTER



Soko lililojengwa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Magomeni Kota Machinga Center.





Kwaya ya **Chuo cha Utumishi wa Umma** ikitumbuiza wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**

Mwimbaji wa nyimbo za Singeli **Seif Mwinyi Juma** Maarufu kama **Sholo Mwamba** akitumbuiza wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Kikundi cha **JKT Ngoma** kikitumbuiza wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Nyumba 644 za Makazi za **Magomeni Kota**.



Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)
Makao Makuu: Barabara ya Sokoine 2,
Mkabala na Ukumbi wa Karimjee
S.L.P 9542 Dar es Salaam, Tanzania



Simu: +255 733 483 437,
+255 677 108 010



Nukushi: +255 22 2114143



Barua Pepe : ce@tba.go.tz
barua@tba.go.tz



Proudly Housing Public Servants in Tanzania



www.tba.go.tz



@WakalaWaMajengoTanzania

